

Jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

NIPASHE UK 10

na wilaya," alisema.

# Serikali yatakiwa kutoa kauli ushuru bidhaa za ngozi

MBUNGE wa Viti maalum, Halima Mdee ameitaka serikali kutoa kauli kuhusu malalamiko ya wadau wa ngozi kuhusu ushuru mkubwa unaozwa bandarini na vikwazo vya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi.

Akijibu swali hilo bungeni jana, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema viwango vya ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi na

ngozi iliyosindikwa kiwango cha kati (Wet blue) nje ya nchi ni makubaliano ya nchi wanchama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema walikubaliana kuwianisha viwango vya ushuru kwa lengo la kuhakikisha viwanda vya ndani vinapata malighafi ya kutosha kuzalisha bidhaa za ngozi.

"Ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi (export levy)

ni asilimia 80 ya thamani ya mzigo ukiwa bandarini (FOB) au Dola za kimarekani 0.52 kwa kilo," alisema.

Alisema ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati zinatozwa ushuru wa asilimia 10 ya FOB ili kutoa motisha kwa wasindikaji.

"Ngozi zilizosindikwa hadi kufikia hatua ya mwisho (finished leather) hazitozwi ushuru wowote (0%). Jitihada hizo

zimesaidia kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi," alisema.

Vile vile, alisema hakuna vikwazo vyovyote katika kusafirisha ngozi, kwa kuwa takwimu zinaonyesha kiwango cha usafirishaji ngozi ghafi kimeendelea kupanda kutoka kilo 513,201 mwaka 2015/16 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/21.



Habari zote na Augusta Njoji



Livestock and Fisheries deputy minister Abdallah Ulega (L) talks with International Centre for Antimicrobial Resistance Solutions Operations Director Helle Engslund Krarup. The discussion centred on how ICARS will facilitate projects to reduce the use of pesticides in poultry keeping in the country held in Dodoma recently. Photo: Guardian Correspondent

# Hides, skin exports surge

EXPORTS of hides and skin have increased from 513.2 tonnes in 2015/16 to about 7,370 tonnes in 2020/21, the government has said.

Deputy Minister for Livestock and Fisheries, Abdallah Ulega said in Parliament yesterday that there were no restrictions on exports of the products.


The Deputy Minister was responding to a question by Special Seats lawmaker, Halima Mdee (CHADEMA) who raised concern that the hides and skin were being charged high levies by authorities at the ports and that there were also complications when it came to exporting the products outside the country.

In his response, the deputy minister said levies for transporting skin outside the country was in accordance with the agreement within the East African Community (EAC) member states in efforts to ensure that there is enough raw materials for local industries.

He said EAC member states duty rate of export on hides and skins is set at 80 per cent on the Free On Board (FOB) or USD 0.52 per kilogramme. He added that they also impose a 10 per cent export levy on wet blue leather.

Mr Ulega said that the efforts have helped the country to attract investment in the leather industry.





Mbarali District Commissioner in Mbeya Region Reuben Mfune launches residential post codes at Reini Street yesterday.  
Photo: Correspondent Grace Mwakalinga

THE GUARDIAN Page 3

# Tanzania's export of raw hides, skins has increased

By Felister Peter Dodoma

encourage value addition and attract local and foreign investors in the leather industry.

Ulega was responding to a question from Special Seats MP, Halima Mdee (CHADEMA) who was concerned that stakeholders in the leather sector have been complaining over high export levies.

The legislator wanted to know the

government plans to provide relief to exporters of raw hides and skins because most of the factories have been closed.

The deputy minister said decisions to impose the 80 per cent export levy on raw hides and skins and 10 per cent on raw blue exports was meant to encourage value addition by local industries.

Countries within the East African Community (EAC) agreed to impose the export levies to protect local firms and enhance productivity in the leather industry. The decision was meant to ensure reliable availability of raw materials to local factories manufacturing leather products, said Ulega.

The 80 per cent export levy on the

sector in the development of the telecom sector in Tanzania.

Airtel, as incoming chairman of MIC Tanzania plc, is expected to provide valuable strategic guidance and stewardship to the company and the

networks and developing successful mobile financial services. AXIAN Telecom ambitions to energize the telecommunications ecosystem in Tanzania with a focus on ensuring a better experience for the customers.

products is equivalent to US \$ 0.52 per kilogramme, stated Ulega, adding that there are no levies charged on finished leather exported to various countries.

He however said that most of the produced raw hides and skins are exported to different countries including Nigeria and Ghana. He said efforts are ongoing to ensure collection

of raw hides and skins produced in rural areas.

Data from the Ministry of Livestock and Fisheries indicates that Tanzania has 33.4 million cattle, 21.3 million goats and 5.65 million sheep, more than 1.85 million pigs, 47.4 million indigenous poultry and other many conventional species such as donkeys and rabbits.

UHURU UK 19.



# Wananchi Kyerwa washauriwa kujikita katika ufugaji

NA ANGELA SEBASTIAN, Kyerwa

WANANCHI wa wilayani Kyerwa, mkoani Kagera, wameshauriwa kujikita katika ufugaji, ili kujiongezea kipato na kuinua uchumi wa taifa.

Ushauri huo ulitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Rashid Mwaimu, alipozungumza na gazeti hili ofisini kwake mwanzoni mwa wiki hii na kuisitiza kuwa wananchi wanapaswa kufuga kutokana na uwepo wa masoko ya mifugo ya uhakika.

"Wananchi wa wilaya hii sasa wana kila sababu ya kuongeza ufugaji na kuwa na tija ili kuinua uchumi wa taifa na kujiongezea kipato maana kwa kipindi cha mwaka huu mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Kyerwa imeanzisha minada miwili

ya mifugo," alisema.

Mwaimu alitaja minada hiyo kuwa ni ya vijiji vya Katera na Murongo ambayo ni fursa kwa wananchi na wanapaswa kuichangamkia ili wajikwamue kiuchumi.

Alieleza kuwa serikali inaendelea kukarabati na kujenga majosho katika mbuga mbalimbali za mifugo wilayani hapa zikiwemo za Luhita na Kababe katika Kata ya Mabira kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kufuga kisasa na kwa tija na kuwapunguzia changamoto zisizokuwa za lazima.

Mfugaji wa Nkwenda, Sudi Nyemenohi, alisema minada hiyo iliyoanzishwa Kyerwa imewasaidia kuuza mifugo yao kwa bei ya juu, ambapo awali walikuwa wakiipeleka nchi jirani ya Uganda na kuiuza kwa bei

ya chini huku wakitembea umbali mrefu kufuata soko.

Nyemenohi aliishukuru serikali ya awamu ya sita kwa kuanzisha minada hiyo ambayo ni ukombozi na kuiomba kuendelea kujengwa majosho ya kutosha ya kuoshea mifugo ili kukabiliana na magonjwa ya kupe.

## OMBI

### UJENZI WA MAJOSHO

Wananchi wa Wilaya ya Kyerwa, wameiomba serikali kuwajengea majosho ya kutosha ya kuoshea mifugo ili kukabiliana na magonjwa ya kupe.

# \* Serikali: Hakuna vikwazo vya usafirishaji zao la ngozi \*

UHURU UK.S.

SERIKALI imesema hakuna vikwazo vyovyote katika kusafirisha zao la ngozi, kwani takwimu zinaonyesha kiwango cha usafirishaji ngozi ghafi kimeendelea kupanda kutoka kilo 513,201 mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/2021.

Kauli hiyo ilitolewa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu (CHADEMA), Halima Mdee.

Katika swali lake, Halima alitaka kujua kauli ya serikali juu ya malalamiko ya wadau wa ngozi kuhusu ushuru mkubwa unaotozwa bandarini na vikwazo vya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema viwango vya ushuru wa kusafirisha ngozi

ghafi na ngozi iliyosindikwa, kiwango cha kati kwenda nje ya nchi ni makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) waliyokubaliana kuainisha viwango vya ushuru kwa lengo la kuhakikisha viwanda vya ndani vinapata malighafi ya kutosha kuzalisha bidhaa za ngozi.

Ulega alisema ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi ni asilimia 80 ya thamani ya mzigo ukiwa bandarini (FOB) au dola 0.52 kwa kilo.

"Ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati zinatozwa ushuru wa asilimia 10 ya FOB ili kutoa motisha kwa wasindikaji. Ngozi zilizosindikwa hadi kufikia hatua ya mwisho hazitozwi ushuru wowote," alisisitiza.

Naibu waziri huyo alisema jitihada

hizo zimesaidia kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi.

"Hakuna vikwazo vyovyote katika kusafirisha zao la ngozi kwa kuwa, takwimu zinaonyesha kiwango cha usafirishaji ngozi ghafi, kimeendelea kupanda kutoka kilo 513,201 mwaka 2015/2016 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/2021," alisema.

## Vikwazo

### NGOZI

Alisema viwango vya ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi na ngozi iliyosindikwa...



usalama pamoja na magari  
yaliyopata kibali maalumu

# \* HABARI LEO UK \* 'Hakuna vikwazo usafirishaji ngozi'

**S**ERIKALI imesema hakuna vikwazo vyovyote katika kusafirisha zao la ngozi kutokana na kuongezeka kwa kiwango cha usafirishaji ngozi ghafi kutoka kilogramu 513,201 mwaka 2015/16 hadi kufikia kilo 7,370,533 mwaka 2020/21.

Hayo yafibainishwa na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu, Halima Mdee (Chadema) aliyetaka kufahamu kauli ya serikali kuhusu malalamiko ya wadau wa ngozi kuhusu ushuru mkubwa unaotozwa bandarini na vikwazo vya kusafirisha bidhaa hiyo nje ya nchi.

Ulega alisema viwango vya ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi na ngozi iliyo-sindikwa kiwango cha kati nje ya nchi ni makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki waliokubaliana kuwianisha viwango vya ushuru kwa lengo la kuhakikisha viwanda vya ndani vinapata malighafi ya kutosha kuzalisha bidhaa za ngozi.

Alisema ushuru wa kusafirisha ngozi ghafi nje ya nchi ni asilimia 80 ya thamani ya mzigo ukiwa bandarini (FOB) au dola za Marekani 0.52 kwa kilo.

Aidha, ngozi zilizosindikwa kwa kiwango cha kati zinatozwa ushuru wa asilimia 10 ya FOB ili kutoa motisha kwa wasindikaji.

"Ngozi zilizosindikwa hadi kufikia hatua ya mwisho hazitowzi ushuru wowote. Jitihada hizo zimesaidia kuvutia uwekezaji katika viwanda vya kusindika ngozi na kuzalisha bidhaa za ngozi," alisema.